Candidate's Number ____________

# THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
## MINISTRY OF EDUCATION AND CULTURE
## FORM TWO SECONDARY EDUCATION EXAMINATION, 1992

0021 KISWAHILI

MUDA: SAA 2.30

---

(a) Jibu maswali yote 13. Majibu ya maswali 1 na 2 yaandikwe katika karatasi utakazopewa. Kisha funga karatasi hizo mwishoni mwa karatasi hii. Majibu ya maswali mengine yaandikwe katika nafasi zilizoonyeshwa katika karatasi hii.

(b) Fuata maagizo ya kila sehemu na ya kila swali.

(c) Kumbuka kuandika namba yako ya Mtihani katika kila ukurasa.

| KWA MATUMIZI YA WATAHINI TU | | |
|---|---|---|
| SWALI | ALAMA | SAINI |
| 1 | | |
| 2 | | |
| 3 | | |
| 4 | | |
| 5 | | |
| 6 | | |
| 7 | | |
| 8 | | |
| 9 | | |
| 10 | | |
| 11 | | |
| 12 | | |
| 13 | | |

Karatasi hii ina kurasa 6 zenye maandishi.

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Scanned with CamScanner

 Candidate's Number ___________

## SEHEMU A : UTUNGAJI

1. Chagua kichwa cha habari kimoja kati ya vifuatavyo na ukiandikie insha ya maneno yasiyopungua 200.

   (a) Michezo shuleni

   (b) Moto na mazingira.

2. Barua ifuatayo ina makosa kadhaa. Iandike upya na kwa usahihi.

Jidonge Maduka
Shule ya Sekondari Nguvumali
S.L.P. 202
Tanga
10-10-1992

Meneja Mkuu,
Kiwanda cha Nyuzi,
S.L.P. 100,
TABORA.

OMBI LA KAZI YA MUDA

Ndugu Meneja,

Shikamoo. Tafadhali husika na kichwa cha habari.

Naomba kupatiwa nafasi ya kazi yoyote ya muda katika kiwanda chako.

Mimi ni kijana wa kiume mwenye umri wa miaka 17. Ninasoma kidato cha pili mkoani Tanga. Hivi karibuni shule itafungwa kwa ajili ya likizo. Nami nategemea kuwa Tabora kuanzia tarehe 01-12-92 hadi 15-01-93. Hivyo ninaomba kufanya kazi katika kipindi hicho kisichopungua mwezi mmoja na nusu.

Salaam nyingi kwa familia yako. Tutaonana siku nitakayoanza kazi.

Ahsante sana.

## SEHEMU B : UFAHAMU NA UFUPISHO

3. Soma habari ifuatayo kwa makini na kisha ujibu maswali yanayofuatia :-

Ah maskini ya Rabi ee hii ndiyo nchi tuliyomo sasa. Ndiyo, ee jasho letu linanunua nywele za maiti ili dada zetu wavae. Jasho letu linanunua maradhi ya kansa. Rafiki zangu endeleeni, yapanueni mambo yetu, pigeni kelele, chekeni, sengenyeni, ungurumeni, muda ukifikia mtanyamaza. Mbuzi atakapo wika, kondoo atakapobweka, mbwa atakapokamua maziwa, ndiyo mwisho wa fisikoko kuwasumbua kondoo, ndiyo mwisho wa mumiani kukamua damu. Hata hivyo si kitu sana kwani mwisho wa yote tanuru la ujamaa lenye mfuniko wa haki litaunguza fisikoko. Kuni za ujamaa zitaendeleza moto. Dunia ni mapishano, wengine ni panya walishwa sumu, wengine ni punda wabeba mizigo, wengine ni ng'ombe wa kulima na kutoa maziwa.

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Scanned with CamScanner

Candidate's Number ____________

Sasa nimechoka kunyanyaswa, nimeamua kupambana kuipigania kiu ya haki, haki isiyotenga kati ya kuku na mwewe, paka na pany, punda na ng'ombe. AH usawa ........ Usawa ......... maana yake nini?

MASWALI:

(a) (i) Andika kichwa cha habari hii.

______________________________

______________________________

(ii) Mwandishi anasema mwisho wa yote kutatokea nini?

______________________________

______________________________

______________________________

(iii) Unafikiri mwandishi analalamika juu ya jambo gani?

______________________________

______________________________

(iv) Mwandishi anasema dawa ya kumaliza uonevu ni ipi ?

______________________________

______________________________

(b) Andika ufupisho wa habari hii kwa maneno yasiyozidi 60..

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Scanned with CamScanner

## SEHEMU C : SARUFI

4. Bainisha aina ya sentensi zifuatazo:-

(a) Daktari aliyemchoma dada sindano amehamia Mbeya.

_______________________________________________

(b) Baba anasoma hadithi na mimi ninasikiliza redio.

_______________________________________________

(c) Kaka akifika kesho tutaondoka.

_______________________________________________

5. Tumia alama K kwa kiima na A kwa kiarifu katika kubainisha kiima na kiarifu katika tungo zifuatazo:-

(a) Mzee Katoto amelazwa hospitalini.

_______________________________________________

(b) Kwa wingi mno, mananasi yalilimwa Ukerewe.

_______________________________________________

(c) Wanacheza mpira kifundi.

_______________________________________________

6. Andika sentensi zifuatazo kwa usahihi :-

(a) Kijana yule aliyosimama pale ni kaka yangu.

_______________________________________________

(b) Mle alikoingia ni shimoni.

_______________________________________________

(c) Watoto ambawo wanacheza darasani hawafaulu mtihani.

_______________________________________________

7. Malizia methali zifuatazo:

(a) Halilala hadingwadingwa _______________________

(b) Mwenda bure _______________________

(c) Chanda chema _______________________

8. Ainisha maneno yaliyomo katika tungo zifuatazo:-

(a) Niliwakuta vijana wanne wanakunywa chai.

_______________________________________________

_______________________________________________

(b) Mtoto huyu angelikuwa anajifunza hangelishindwa.

_______________________________________________

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Scanned with CamScanner

Candidate's Number ______________

## SEHEMU D : FASIHI SIMULIZI

9. Katika hadithi za fasihi simulizi lazima yawepo mambo manne ili hadithi ikamilike :-

(a) ______________

(b) ______________

(c) ______________

(d) ______________

10. Taja wahusika wakuu (3) wa fasihi simulizi :-

(a) ______________

(b) ______________

(c) ______________

11. Eleza shabaha ya kila mojawapo ya mambo yafuatayo ya fasihi simulizi :-

(a) Tambiko katika jamii ______________

(b) Miviga katika jamii ______________

(c) Utani katika jamii ______________

(d) Vitendawili katika jamii ______________

(e) Methali katika jamii ______________

12. (a) Kitendawili ni nini? ______________

______________

(b) Tegua vitendawili vifuatavyo :-

(i) Nilikwenda kwa rafiki yangu tuko wawili. Nilipokaribishwa nyumbani niliingia peke yangu, rafiki yangu akabaki mlangoni

______________

(ii) Nililima shamba kubwa, nilipovuna nilijaza kiganja tu.

______________

(iii) Niliamka, unga wangu asubuhi sikuukuta

______________

(iv) Chukua ungo, wewe na mimi tupepete kisichopepeteka.

______________

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Scanned with CamScanner

Candidate's Number ____________

13. Ifuatayo ni sehemu ya majigambo ya mtambaji fulani. Isome kwa makini na kisha jibu maswali yanayofuatia:

(a) Ugumu wa kuchonga mzinga tena wa mninga,
Ugumu wa kurina asali - Ah hii ndiyo asali,
Miiba ya machungani, tena wakati wa mvua.
Ugumu wa kukamua, ng'ombe walio wakali,
Ah - haya ndiyo maziwa!

(b) Hivi ndivyo yalivyo, nani atakayetuokoa,
Ni sisi wenyewe,
Tukate,
Tufyeke,
Tung'oe
Na kutupilia mbali ha! ha! ha!

(c) Upepo!
Upepo mwanana,
huu upepo wa matumaini,
Tunauombea ulete kheri,
Kheri ilo kheri,
Kheri ya matumaini,
Kheri iso waa,
Kheri ya milele.

MASWALI:

(a) Mtambaji ana ujumbe gani?

______________________________

______________________________

______________________________

(b) Je, mtambaji anatamba wakati wa furaha au majonzi? Kwa nini?

______________________________

______________________________

(c) Unafikiri mtambaji anaridhika na hali ya maisha iliyopo? Kama ndivyo au sivyo kwa nini?

______________________________

______________________________

______________________________

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Scanned with CamScanner